Pg 7.

# TRC yaanza rasmi kuunda vichwa vya treni za MGR nchini

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limeanza rasmi kuunda vichwa vya treni za Reli ya MGR nchini, hatua inayolenga kupunguza gharama za uagizaji wa vifaa hivyo kutoka nje na kuongeza ujuzi kwa wataalamu wa ndani.

Hatua hiyo imekuja baada ya vichwa viwili vya treni kati ya vinane vya daraja la 91XX kuundwa katika karakana ya TRC iliyopo Dar es Salaam kupitia mradi wa uundaji wa vichwa vya treni za MGR.

Akizungumza baada ya kukagua karakana hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso aliitaka Wizara ya Uchukuzi kupitia TRC kuendelea kuwajengea uwezo vijana wa Kitanzania wanaohusika katika uundaji na ukarabati wa vichwa hivyo kwa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu ndani na nje ya nchi.

Alisema ni muhimu kuwapeleka wataalamu hao kupata ujuzi na utaalamu zaidi ili kuongeza ubunifu na ufanisi katika kazi wanazozifanya.

"Wizara na TRC hakikisheni mnawapeleka vijana hawa nje ya nchi ili wakajifunze na kuchota utaalamu zaidi. Waliopo hapa pia wapewe kipaumbele na wale waliobobea zaidi waboreshewe maslahi yao ili waendelee kulitumikia shirika na taifa kwa uaminifu," alisema Kakoso.

Aliongeza kuwa uamuzi wa TRC kuanza kuunda vichwa vya treni hapa nchini umeipunguzia serikali gharama ambazo zingetumika kununua vifaa hivyo nje ya nchi, huku pia ukitoa ajira kwa vijana na kuwapa nafasi ya kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa taifa.

Aliitaka TRC kuhakikisha karakana hiyo inafanya kazi usiku na mchana ili kuendana na mahitaji ya soko na kuhakikisha upatikanaji wa vichwa vya treni kwa wakati.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile alisema serikali inaendelea kukuza sekta ya uchukuzi kwa kuimarisha miundombinu ya reli na kununua vitendea kazi muhimu, ikiwemo vichwa na mabehewa ya treni.

Alisema serikali imeendelea na ujenzi wa reli ya kisasa kwa zaidi ya kilometa 2,000 na inaendelea kununua vifaa vya reli ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji nchini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Machibwa Shiwa alisema kuanza uundaji wa vichwa vya treni nchini utapunguza muda na gharama za kuagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Aliongeza kuwa TRC ina mkakati wa kushirikiana na sekta binafsi ili kuweza kuunda vichwa takribani 30 kwa mwaka, hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi na kuhakikisha upatikanaji wa vichwa vya treni kwa wakati.

TRC iliingia mkataba na Kampuni ya SMH Rail ya Malaysia Oktoba 24, 2022 kwa ajili ya uundaji wa vichwa vipya vya treni za MGR nane vya daraja la 91XX.

Kati ya vichwa hivyo, viwili vilitengenezwa Malaysia wakati vingine sita vikitarajiwa kuundwa nchini Tanzania ambapo hadi sasa viwili kati ya hivyo tayari vimekamilika.

CS CamScanner